

102/1

**KISWAHILI**

**KARATASI YA 1**

**(INSHA)**

**KIDATO CAH TATU.**

Mwongozo wa ksahihisha ni mali ya barasa la mtihani la tathmini ya pamoja ; eneo la ugatuzi la Trans-Nzoia

**SWALI LA KWANZA**

Ni swali la onyo au ilani. Sura lazima izingatiwe

HOJA.

1. Mtahiniwa haruhusiwi kuiingia katika chumba cha mtihani akiwa na simu/rununu
2. Wasimamizi hawafai kuingia na rununu katika chumba cha mtihani
3. Wasimamizi wakuu wa mitihani na walimu wakuu wa shule pekee yao wanaruhusiwa kuwa na simu lakini ni kwa minajili ya mawasiliano kwa waziri wa elimu, mkuu wa elimu wilayani, mkurugenzi wa elimu mkoani ama halmashauri ya mitihani nchini Kenya(KNEC)
4. Msimamizi mkuu wa mitihani na mwalimu mkuu hawatakikani katika chumba/vyumba vya mitihani wakiwa na rununu zao
5. Mawasiliano ya karatasi za maswali hayafai kukaguliwa na mwalimu mkuu wala mwalimu yeyote kabla wa muda wa mtihani huo kukamilika
6. Msimamizi mkuu haruhusiwi kutoa masalio ya karatasi za maswali katika chumba cha mtihani
7. Wasimamizi wanafaa kuifunga bahasha ya maswali na kkuweka mbele ya chumba cha mtihani
8. Ni hatia kwa mtahiniwa kuingia katika chumba cha mtihani na kifaa chochote kisichohitajika kama vile nakala za kusoma, vitabu vya maandalizi, na majibu yoyote ya mtihani
9. Ni hatia kwa mtahiniwa kubeba karatasi bila maandiko katika chumba cha mtihani au maelekezo ya kikokotozi au kifaa chochote kitakachomwelekeza mtahiniwa.
10. Ni hatia kwa mtahiniwa kujihami katika chumba chaa mtihani na/au kikokotoo kilicho na maelekezo au kifaa chochote kitakachomsaidia kudnaganya

11. Ni hatia kwa watahiniwa kusaidiana kujibu maswali ya mtihani
12. Ni hatia kwa mtu yeyote kufanya mtihani kwa niaba ya mtahiniwa mwenyewe
13. Mtu yeyote atakayepatikana na hatia ya kuzingatia kanuni hizi atakuwa amekiuka kanuni za halmashauri ya mitihani ya kitaifa nchini na atachukuliwa hatua kali.
  - a. Kuvunja sheria au kanuni 1,8, 10 na 11 ; matokeo ya mtahiniwa katika somo husika yatatupiliwa mbali na atatuzwa alama 'Y' hivyo alama yake ya matokeo itakuwa 'Y' na kisha hataruhusiwa kufanya mitihani minane ya KNEC kwa miaka miwili.
  - b. Kuvunja kanuni ya 2, 3, 4, 5, 6 na 7 ; watashtakiwa na wakipatikana na hatia wataachishwa kazi.
  - c. Kuvunja kanuni ya 12 ;(Kufanya mtihani kwa niaba) mtahiniwa atatiwa mbaroni au kushtakiwa na kulipa faini.

### **KUTUZA**

Tahadhari zake ziwe zaidi ya 7 kisha atoe hatua 3 muhimu zitachukuliwa

Akitaja tahadhari pekee akadiriwe kwa kiwango cha C+(Alama 10)

Akitaja hatua pekee bila kuzongatia tahadhari atakuwa amejitungia swali(Kiwango cha D-)

### **SWALI LA PILI**

Thibitisha : Ni kutoa maelezo yenye kudhihirisha kuwa linalosemwa ni la ukweli au si la ukweli.

Uhuru wa vijana

Hoja za kuunga mkono

1. Vijana wametengewa nyadhifa za uongozi katika ngazi za ugatuzi
2. Vijana huchagua viongozi wao wa kisiasa
3. Vijana wameruhusiwa kutoa maoni yao katika maswala ya kijamii
4. Vijana huruhusiwa kujiunga na kundi lolote la kidini kukuza imani yao
5. Vijana wana uhuru wa kujiunga na makundi au mashirika ya kuwawezesha kutwaa mikopo ya fedha kutoka katika hazina ya vijana
6. Vijana wana uhuru wa kutangamana na wale wawapendao
7. Vijana wana uhuru wa kuchagua wa kuoa au kuolewa ili kuanzisha familia
8. Vijana wana uhuru wa kujichagulia taaluma za kusomea

9. Vijana wana uhuru wa kukuza vipawa vyao kwa kushiriki mashindano iliwa katika ngazi zote kuanzia mashinani hadi kitaifa kama vile mashindano ya riana, kanda, muziki ili kushindania tuzo tofauti.

Hoja za kupinga

Vijana hawana uhuru wa kushiriki mambo yafuatayo.

- i) Kutumia vileo au dawa za kulevya
- ii) Kuvalia mavazi yasio na adabu/heshima
- iii) Kuiga kikasuku desturi za kigeni
- iv) Kutazama au kusoma filamu au fasihi ghushi
- v) Kushiriki ukahaba au ushoga
- vi) Kushiriki burudani au tafrija katika majumba ya starehe
- vii) Kushiriki mapenzi nje ya ndoa
- viii) Kushiriki katika ujambazi, wizi na ugaidi

KUTUZA

Akidhihirisha ni ukweli au si ukweli atoe hoja zote

SWALI LA TATU

Ni swali la methali

Abainishe maana ya ,ethali kisha atungie kisa kimoja kinachothibitisha methalli hio

Maana: Jambo lisilokuhusu linakukera kivipi au kwa njia gani?

Ni vyema kutoingilia mambo yasiyotuhusu na yanayoweza kutuleta matatizo. Kwa mfano ugomvi au vita kati ya watu wawili.

KUTUZA.

Methali huwa na pande mbili. Asipojihusisha na pande zote mbili amejitungia swali lake mwenyewe na kulijibu.

Akitoa kisa kisichooana na methali yenyewe atakuwa amejitungia swali

Swali la mdokezo

- i) Lazima mtahiniwa amalizie kwa mdokezo huu. Asipofanya hivyo amejitungia swali.
- ii) Akipunguza idadi ya maneno katika mdokezo amejitungia swali
- iii) Akiongezea maneno matano au zaidi baada ya mdokezo, atakuwa amejitungia swali

Kisa kilenge kufunza mtu anaweza kuwa amezaliwa katika jamii maskini lakini ajibidishe kimaisha na awe tajiri

Au

Mtu asisitikie hali yake ila afanye biddii kuirekebisha

